

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A

610

UALIMU

Muda: Saa 3

Jumanne, 10 Mei 2011 Asubuhi

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A na swali **moja (1)** kutoka kila sehemu B, C, D na E.
3. Sehemu A ina alama 40, sehemu B, C, D na E zina alama 15 kila moja.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha **kujibia**.

Karatasi hii ina kurasa 4 zenyе maandishi.

SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Eleza kwa kifupi changamoto nne zinazoifanya kazi ya ualimu hapa Tanzania ionekane ni kazi ngumu na isiyo na mvuto.
2. Orodhesha mbinu nne za jinsi ya kumsaidia mtoto aliyevia akili katika kujifunza.
3. Bainisha mambo manne ambayo mwalimu anapaswa kuyafanya wakati wa ufundishaji iji kuwezesha darasa lake kuwa na nidhamu.
4. Tofautisha utafiti wa saveyi na utafiti wa kisamafunzo.
5. Orodhesha sifa nne zinazoonesha kufanana kwa elimu ya jadi na elimu ya kujitegemea.
6. Eleza kwa kifupi sababu nne zinazowafanya baadhi ya wanafunzi kuwa na hofu ya kutafuta huduma ya ushauri nasaha kutoka kwa walimu wao.
7. Eleza sababu za kufanya tathmini zifuatazo katika elimu:
 - (a) Tathmini endelezi.
 - (b) Tathmini dodoso.
8. Taja faida nne za mazoezi ya kufundisha kwa mwalimu mwanafunzi.
9. (a) Eleza dhana ya hisa ya akili kama ilivyofafanuliwa na mwanaasaikolojia Alfred Binet.
(b) Andika kanuni ya kukokotoa hisa ya akili.
10. Bainisha njia mbili zinazoweza kutumika katika kuwabaini wanafunzi wenye mahitaji maalum.

SEHEMU B: SAIKOLOJIA YA ELIMU (Alama 15)

Jibu swali **moja (1)** kutoka katika sehemu hii.

11. Eleza kwa ufasaha kuhusu nyanja ya utambuzi pamoja na vipengele vyake vyote.
12. Ramadhani ni mionganini mwa wanafunzi waliowekwa kwenye kundi la watoto waliovia akili kwa vile ana kichwa kikubwa. Andika hoja tano za kisaikolojia kuonesha kuwa Ramadhani amepangwa katika kundi hilo kimakosa.

SEHEMU C: MITAALA NA UFUNDISHAJI (Alama 15)

Jibu swali **moja** (1) kutoka katika sehemu hii.

- ✓ 13. Kwa kutumia hoja tano jadili mambo makuu yanayoweza kusababisha mtaala kubadilika katika mfumo wa elimu.
- 14. Fafanua mambo muthimtu sita yanayopaswa kuandikwa kwenye kumbukumbu za maendeleo ya wanafunzi.

SEHEMU D: UTAFITI WA KIELIMU, UPIMAJI NA TATHIMINI (Alama 15)

Jibu swali **moja** (1) kutoka katika sehemu hii.

- 15. Chunguza alama za wanafunzi walizopata katika somo la Elimu kwa Michezo kisha jibu maswali yafuatayo:

Mtaahiniwa	A	B	C	D	E	F	G	H	I	J	K	L
Alama	75	63	57	65	52	78	55	65	59	62	63	65

- (a) Tafuta achano sanifu. Tumia:

$$AS = \sqrt{\frac{\sum(X - \bar{X})^2}{N}}$$

- (b) Achano sanifu liliopatikana linamaanisha nini?
- (c) Rekebeishwa alama walizopata watahiniwa F na E.
- (d) Alama zilizorekebishwa kwa kigezo cha "T" ni bora zaidi kuliko kigezo cha "Z." Toa sababu.
- (e) Wapang'e wanafunzi kwa nafasi kwa kutumia alama ghaffi.

- 16. ✓ Utafiti wa matumizi ni bora zaidi kuliko utafiti wa msingi hasa katika suala la maendeleo ya elimu. Fafanua kauli hii kwa kutumia hoja tano (S).

SEHEMU E: MISINGI YA ELIMU (Alama 15)

Jibu swali **moja (1)** kutoka katika sehemu hii.

17. ✓ Kwa kutumia hoja sita eleza jinsi ya kuwasaidia wanafunzi **wenye mahitaji maalum** katika shule unayofundisha.
18. Umeteuliwa kuwa mwalimu mkuu wa shule ya msingi Jitegemee. Fafanua kwa kutumia hoja sita jinsi utakavyotumia uongozi wa kidemokrasia **kuongoza** shule hiyo.